ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.

14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini

32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34 .Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg. Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hati ya Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na kuweka masharti bora ndani yake. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na kuweka masharti bora ndani yake. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 72

Semina za Baraza la Wawakilishi Kutofanyika Bwawani

Mhe. Salim Abdulla Hamad - Aliuliza:-

Tumeshuhudia kuwa Semina nyingi zinazofanyika ambazo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hushiriki hufanyika katika mahoteli ya watu binafsi badala ya Hoteli ya Bwawani ambayo ni yenye nafasi nzuri na ingeweza kufaidika na kujipatia fedha nyingi za kodi. Kwa nini Baraza la Wawakilishi likawa linaamua hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 72 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hushiriki kwenye semina nyingi ambazo hazifanyiki kwenye Hoteli ya Bwawani, jambo hilo limechangiwa na sababu mbali mbali zifuatazo:-

i. Mhe. Spika, katika mfumo wa uhuru wa kibiashara na ushindani wa soko unaruhusu taasisi kuchagua pale ambapo atapata huduma bora na unafuu wa bei (*value for money*).

ii. Mhe. Spika, kwa sababu kuna watu wengine huomba huduma za semina na huduma nyengine kutoka Hoteli ya Bwawani hivyo husababisha mteja mwengine kukosa nafasi ya kupata huduma hiyo kwa wakati unaohitajika hivyo inabidi kutafuta sehemu nyengine ya kufanya shughuli yake kwa wakati huo.

iii. Mhe. Spika, wakati mwengine Taasisi inayotoa semina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi huandaa sehemu ya kufanyia semina hiyo, tunachozingatia ni kupata huduma bora inayoendana na hadhi ya Baraza.

iv. Mhe. Spika, zipo semina ambazo waheshimiwa wenyewe huomba zifanyike nje ya mji kwa sababu ya kuleta utulivu kwa wajumbe ili waweze kufanya shughuli zao vizuri. Kutokana na sababu hizo ndio hupelekea kufanya semina zetu katika sehemu ambayo inakidhi haja ya mahitaji yetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Waziri alipokuwa akijibu jibu la msingi amesema kwamba waandaaji wa semina hizo hufuata mahoteli kulingana na huduma nzuri kuliko hoteli yetu ya Bwawani. Mimi naomba kujua ni huduma

zipi ambazo hutolewa katika mahoteli mengine ambapo Hoteli ya Bwawani hazipo zinazosababisha wawakilishi kuzikataa.

b) Pia naomba kujua kuna tofauti gani ya bei kati ya hoteli ambazo Baraza hili hufanyia semina hata zikawa ni bora zaidi kuliko bei za Hoteli ya Bwawani kwa uoni wangu ni za chini na zinasaidia sana hoteli ile.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, sote ni wazoefu wa Hoteli ya Bwawani na hali yake tunaijua, wakati mwengine vifaa ambavyo vya kufanyia shughuli unayoitaka pengine huwa vina upungufu wa kwenda kufanya shughuli hiyo. Vile vile mheshimiwa kama nilivyosema ni uamuzi wa taasisi husika au mteja anayetaka kufanya ile shughuli analinganisha, akiona niende Bwawani huduma zangu zitakuwa zinakidhi tunachukua, tukiona huduma hazikidhi kwa shughuli hiyo hatufanyi, tunafanya pale ambapo tunaona patatosheleza haja.

Mhe. Spika, hivi karibuni tulipotaka kuamua kufanya ile Semina ya Mafunzo kwa ajili ya Uandishi wa Sheria. Ni kwamba tulikwenda Bwawani wahusika ni *UNDP* walikwenda huko Bwawani wakenda na mahoteli mengine baada ya kutafakari bei, bei ya Bwawani ilikuwa ni kubwa kuliko bei ya *Neptune*. Kwa hivyo, ndio ukatolewa uamuzi wa kwenda kule *Neptune*, sisi sio kwamba tunakataa Bwawani, lakini nataka niseme wazi Mhe. Spika, kwa hali ilivyo ya Bwawani inahitaji mabadiliko makubwa. Inahitaji mabadiliko ya kiujenzi, inahitaji mabadiliko ya kiutendaji, inahitaji mabadiliko ya yale mazingira yenyewe ilivyo haiwezi tena kuendelea hali ile ikawa ni jaa la mbu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu yake Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa Bwawani kuna kumbi mbili ambazo ni nzuri, wapishi wake wanapika chakula kizuri. Pia Mhe. Waziri huoni kuwa wewe ni Waziri na unasema kwamba ile Hoteli ya Bwawani haina kiwango hivyo huoni kama unaishushia hadhi Hoteli ya Bwawani ambayo ni ya serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, tumesema hapa tutasema ukweli na tumeapa kusema ukweli, hivyo mimi nitasema ukweli kwamba hadhi ya Hoteli ya Bwawani haifikii kiwango ukilinganisha na mahoteli mengine, ni wajibu wetu tuiendeleze na Serikali imeamua hilo kuiendeleza Hoteli ya Bwawani na hivi karibuni mtasikia namna gani itakavyoendeleza Bwawani, sio kama hali ile.

Mhe. Asha Bakar Makame: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku ya leo kuamka salama. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametujibu majibu mazuri si mabaya na nakubaliana na baadhi ya mambo. Lakini kwa kuwa Bwawani ni miongoni mwa taasisi ya Serikali, na kwa kuwa Bwawani kila siku inapigwa ticktaka mara mkodishaji huyu, mara mkodishaji huyu mpaka tukasema irudi katika mikono ya taasisi ya Serikali.

Je, atalihakikishia vipi Baraza hili tukufu kwa kipindi hiki kinachokuja cha bajeti kwamba watahakikisha Bwawani kwa sababu ndio rasilimali iliyobakia ya serikali, atahakikisha kwamba Bwawani inachukua hadhi kama mahoteli mengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, Serikali imeamua kufanya mabadiliko makubwa kuhusu Hoteli ya Bwawani, hivi sasa imeunda kamati maalum ya Baraza la Mapinduzi kushughulikia suala hilo na taratibu zinaendelea kwa nia ya kuleta mabadiliko makubwa kwenye Hoteli ya Bwawani na sehemu yenyewe ya Bwawani ili tulete maendeleo ya kisasa. Sitaki nimuhakikishie kwamba itakuwa katika kipindi hiki cha bajeti, lakini nia ya Serikali ni kufanya shughuli hizo, na shughuli za pale zitakuwa kubwa Mhe. Spika, kwani zitakapoanza zitachukua muda. Kwa hivyo, napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba mabadiliko makubwa yanakuja.

Mhe. Spika, nataka niseme kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba wakati mwengine tunapoomba kufanya shughuli pale Bwawani huwa tayari kuna mteja mwengine hatupati ile nafasi ndio maana huamua kufanya mahala pengine. Kwa sababu zipo hoja nyingi zinazotokea kwa Hoteli ya Bwawani, sio kwamba tumeidharau moja kwa moja. Mhe. Spika, wakati mwengine huenda tukaomba, na wakati tunapokwenda huwa kuna mteja mwengine kwa msingi huo tunakwenda mahala pengine ili tufanye shughuli zetu. Huo ndio ukweli Mhe. Spika.

Nam. 134

Choo Kinachotumika Kufichua Madawa ya Kulevya

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa choo maalum kwa watu wanaoficha dawa za kulevya, kilichowekwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume, bado hakijaanza kutumika huku kukiwa na taarifa mbali mbali za kuingizwa kwa dawa za kulevya nchini :

(a) Je, kuna sababu zipi zinazopelekea choo hicho kuchelewa kufungwa na kutumika hadi leo.

(b) Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba kuchelewa kufungwa na kutumika kwa choo hicho kunazorotesha juhudi za kupambana na madawa ya kulevya nchini.

(c) Ni lini Serikali itahakikisha choo hicho kimefungwa na kuanza kutumika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 134 lenye kifungu (a), (b) na (c) na kwa vile maswali yanashabihiana kwa hivyo naomba swali (a na b) nijibu kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a+b) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli muda mrefu choo maalum kinachotumika kwa watuhumiwa wa dawa za kulevya bado hakijaanza kutumika, lakini napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa choo hicho hivi sasa tayari kimefungwa katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar lakini bado kunahitajika vifaa vichache ili ufungaji wake ukamilike.

Ni kweli kwamba choo hicho kitakapoanza kutumika kitarahisisha kazi za Jeshi la Polisi katika kuwakamata watuhumiwa, lakini hata hivyo, kutokukamilika kwake hakukuzorotesha mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa vile kazi hizo zinaendelezwa kwa kutumia njia mbadala.

(c) Jeshi la Polisi ndilo ambalo linajukumu la kuhakikisha kwamba choo hicho kinakamilika kufungwa na kuanza kutumika rasmi. Kutokana na mawasiliano yetu na Jeshi la Polisi, wameahidi mara tu watakapopata fedha watakamilisha jukumu hilo. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa suala hili, OMPR tayari imewataka Jeshi la Polisi kupeleka bajeti inayohitajika kwa ajili ya kukamilisha shughuli hiyo ili fedha hizo zitolewe kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kukamilisha ujenzi huo haraka iwezekanavyo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, katika kujibu swali hili Mhe. Waziri alisema ni kweli choo hakitumiki lakini pamoja na hivyo kuna njia mbadala. Mimi ningeliomba kujua njia hii mbadala inayotumika inashabihiana kwa kiasi gani na madhumuni ya kujenga choo kile.

b) Ni muda gani mpaka hivi sasa tokea choo kiharibike na umuhimu wa choo hiki ni lini hasa kitaanza kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi asogee karibu na *mic* yake imenipa tabu kusikia masuala yake.

Mhe. Spika : Anauliza njia hiyo mbadala inashabihiana na hiyo ya kutumia hicho choo, hilo la kwanza. La pili ni muda gani hicho choo kimechukua tangu kuwa hakifanyi kazi kwa sababu hizo mbali mbali.
Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, naomba nieleze kwanza kazi ya choo kile ambacho kimefungwa pale na halafu nieleze hiyo njia mbadala nina hakika kwamba tutaelewa kwa kiasi gani zinashabihiana. Kazi ambayo inahitajika kufanywa na choo kile ambacho kinafungwa katika Uwanja wa Ndege ni

pale ambapo tumeshatambua au tumemtuhumu kwamba mtuhumiwa fulani ana dawa za kulevya ndani ya tumbo lake. Kwa hivyo, choo kile kitatumika kwa kumtaka yeye kila anaposikia haja atumie choo kile, na unapotumia katika choo kile dawa zinakaa upande mwengine na choo cha kawaida kinakwenda upande mwengine na hakuna ushughulikiaji wa kutumia mikono ya mwanadamu katika kubagua shuku hiyo, hiyo ndio kazi kubwa ya choo kile kilichofungwa katika uwanja wa ndege.

Sasa kwa kukosekana choo hicho na pia katika nchi nyengine ambazo hawana choo hicho huo ni utaalam mpya, shughuli hii imekuwa ikifanywa kwa kutumia mikono ya mwanadamu, mtuhumiwa anatumia mabeseni katika kwenda haja na utaalam unatumika wa akili za kuzaliwa za mwanadamu katika kutenganisha dawa na choo cha kawaida. Kwa hivyo, hakuna uhusiano wa moja kwa moja isipokuwa kazi inayofanyika inashabihiyana ya kutenganisha dawa na choo kile cha mtuhumiwa.

Kuhusu suala lake la pili sina data kamili hasa choo kile kilianza kufungwa pale lini, lakini ni muda mrefu sana na ndio maana utaona kwamba Serikali imeingilia kati kuwataka Jeshi la Polisi sasa kama wao hawana bajeti ya kukamilisha suala lile, basi Serikali ya Mapinduzi imechukua jukumu ili kuweza kukamilisha na kuweza kurahisisha shughuli hiyo vizuri zaidi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuwepo kwa choo hicho mtu mwenye dawa za kulevya au mtuhumiwa wa dawa za kulevya huwa anachunguzwa kitaalam ili kujulikana kwamba dawa anazo. Na kwa kuwa njia mbadala inayotumiwa mara nyingi tunaweza kusema ni ya kujaribu na kupapasa au kubahatisha, jambo ambalo linaweza kuchangia ongezeko la dawa za kulevya hapa Zanzibar, jambo ambalo kwa kasi kikubwa linaathiri nguvu kazi ya nchi hii, kwani vijana wengi wanakuwa mateja.

a) Je, Mhe. Waziri haoni kwamba gharama za kutengeneza choo kile ni ndogo ukilinganisha na madhara makubwa wanayopata vijana wetu katika nchi hii.
b) Je, kuendelea kuwasubiri Jeshi la Polisi na SMZ kuchelewa kusubiri kwamba SMT watengeneze choo kile huku vijana wetu wakidhalilika huko si kuidhalilisha Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo tumeipata kwa tabu nchi hii.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Naomba nichukue fursa hii tena Mhe. Spika, kufahamisha kazi inayofanywa na choo kile inaonekana waheshimiwa bado hawajaelewa vizuri kazi inayofanywa na choo kile ambacho kinafungwa Air Port si kuweza kutambua kwamba mtuhumiwa ana dawa au hana. Kazi ya kutambua inafanywa kwa vyombo vya *x-ray* baada ya kwisha kutambua sasa pale anapotaka dawa zile zitoke anakwenda haja. Kwa hivyo, choo kile ndio kinachotumika kwa mtuhumiwa kupelekwa kwenda haja chini ya ulinzi, anapokwenda haja bila ya shaka dawa zinatoka na mchanganyiko wa choo cha kawaida cha mwanadamu kazi ya choo kile ni kutenganisha choo cha kawaida na dawa zile.

Sasa shughuli mbadala au njia mbadala inayotumika nimeeleza hapa kwamba watuhumiwa hivi sasa wale ambao nimewataja jana wamekamatwa wale na wakatiwa pipi zile wanapelekwa katika chumba maalum ambacho kina mabeseni tena chini ya ulinzi mkali, hivyo wanatakiwa kufanya haja katika mabeseni hayo na kila wakati inakuwa *observed*. Kwa kweli hakuna upotevu wowote kama kweli mtuhumiwa ana dawa, basi dawa zitaonekana tofauti iliyopo ni jinsi gani tunawashughulikia ule utenganishaji wa dawa na choo kikubwa. Pia nakubaliana na kwamba fedha inayohitajika kuipata pale sio kubwa sana na ni vizuri tukaweza kukitengeneza hiki choo kwa ajili ya kufanikisha shughuli zetu.

Mhe. Spika, suala la pili la Mhe. Mwakilishi anasema kwamba kuisubiri Serikali ya SMT itenge bajeti kwa ajili ya kukamilisha. Mhe. Spika, katika kujibu jibu langu mama nimeeleza kwamba hivi majuzi tu kwa kuona umuhimu na kutaka shughuli ile ikamilike na kuwarahisishia kazi wale wanaofanya kazi kwa kutumia njia mbadala.

Serikali ya Mapinduzi imekubali kubeba gharama hiyo chini ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na nataka nitoe taarifa kwamba hata ule ufungaji wa mwanzo wa choo hiki umefanywa kwa kutumia fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati Jeshi likiwa limebanwa sana na bajeti yake. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitadhalilishwa na tayari imejitolea katika kukamilisha kazi hiyo.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, napenda nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, hapa hiki choo kinachojengwa ni wale watuhumiwa wa dawa wanaokuwa wanaozimeza katika tumbo, na hizi dawa tunasikia zinapita kwa njia nyingi wengine wanazisukia kwenye nywele, wengine wanapasua miili yao wakavitia vidonge. Je, kutakuwa na utaratibu gani kuweza kuzigundua dawa nyengine zitakazokua katika viungo vya binadamu kuliko hii wanayomeza katika tumbo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa kweli nikimwambia hasa njia inayotumika nitakuwa nakisia kisia na sitakuwa na ule ukweli wenyewe kwa sababu hii ni shughuli ya kitaalamu, isipokuwa katika baadhi ya nchi kuna *machine* ambazo mtuhumiwa kama atapita atakuwa anazo hizo dawa basi *machine* ya *x-ray* itaonesha. Hapa nataka tuelewe kwamba zile machine za kawaida haziwezi kuonesha dawa kwa sababu zile sana zinatambua vyombo vya *metal.* Kwa hivyo, dawa hasa kama zikifungwa katika vyombo vya plastik zinaweza kupita au katika mwili wa mwanadamu, lakini wenyewe hasa wataalamu wa shughuli hii kwa kumuangalia yule mtu mwenyewe tayari wanaanza kumshuku kwamba mtu huyo ana dawa katika kitu ambacho amebeba au katika mwili wake. Kwa sababu sisi tumefahamishwa lakini sio vitu vya kuvitoa hapa kwani wenyewe wakisikia huko wataanza kujirekebisha.

Nam. 20

Tatizo la Upatikanaji wa Maji

Mhe. Mohammed Said Mohammed - Aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la maji limekua kubwa na kwa kua baadhi ya miradi ya maji haikufikia malengo ikiwemo *ADB* na *JICA.*

Je, Serikali kwa sasa ina mpango gani madhubuti wa kuondoa tatizo la maji Mjini na Vijijini ili kuwapatia wananchi wake maji bila ya matatizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kutokukubaliana na Mhe. Mwakilishi kwa hoja yake kama inavyojieleza katika swali mama. Napenda kutoa ufafanuzi juu ya hoja kwamba Mradi wa *ADB* upo katika hatua za awali za utekelezaji na kwa hivi sasa uko katika hatua za utoaji wa zabuni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji mijini na vijijini Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mradi wa *JICA* umefikia malengo yaliyokusudiwa, mradi huo kwa kukamilisha ujenzi wa matangi manne, uchimbaji visima, ulazaji mabomba makubwa na ya kati. Aidha, suala la kutokuridhishwa kwa hali ya upatikanaji wa maji nchini kutokana na kushuka mno kwa uzalishaji wa vyanzo vilivyokuwepo awali vilivyosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa katika ulimwengu ikiwemo Zanzibar. Kuharibika kwa mfululizo kwa mitambo ya kusukumia maji, uchakavu wa mtandao wa usambazaji maji katika miji yetu, ujenzi holela uliokithiri katika vyanzo vya maji na mitambo ya maji, pia ujenzi holela wa mahodhi ya chini ya ardhi ambayo mengi yao hayakujengwa kitaalamu na mengi yao yanavujisha maji katika ardhi.

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na juhudi mbali mbali za kuwapatia wananchi wa mijini na vijijini huduma ya maji safi na salama. Mhe. Spika, kukamilika kwa miradi hiyo yote kutapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la maji nchini.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa kwa kuwa amekiri kwamba uzalishaji wa maji sasa ni mdogo Zanzibar, na kwa kuwa nchi za wenzetu sasa duniani ikiwemo Israel imefanya utafiti wa kutumia njia ya upepo na kupata maji kupitia mashine ya *Hydrogate.*

Je, wizara yako ina mkakati gani sasa wa kufanya utafiti wowote ili kupunguza hali hii ngumu inayoukabili umma wa Wazanzibari wote.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kwamba inaliondoa tatizo la maji mijini na vijijini, katika jitihada ambazo inajitahidi ni kuimarisha miradi na kufanya utafiti kama huo aliioueleza, ili kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suala la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri atakubaliana na mimi kwamba kuna kijiji katika shehia yangu kule mpaka sasa hivi wamechangishwa pesa za ulipaji wa maji Vuga Mkadini, na walitegemea kuwa mradi wa *ACRAA* ndio utakaoweza kuwaondolea tatizo lile lakini mpaka leo hii mradi huo haujaanza kufanya kazi.

Je, Mhe. Naibu Waziri una mpango gani wa kuweza kuwarejeshea pesa zao wale wananchi au kuwapatia maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji haimchangishi mtu yeyote yule ambaye hapati maji, isipokuwa wizara yangu humchangisha yule ambaye anapata maji, na hao kama hawapati maji basi wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji itaelekea katika kijiji hicho na kujitahidi tatizo hilo kuliondoa, nao wapate maji safi na salama.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika kwa kunipa fursa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Katika kuwatatulia wananchi wa Zanzibar tatizo la maji, serikali imeleta miradi mbali mbali ili kukuza na kuendeleza maji, ili wananchi wafaidike na maji safi na waondokane na matatizo.

Lakini Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kuwa, kuna sehemu ambazo wananchi walikuwa wanapata maji kwa wingi, lakini katika kuja miradi hii ndio sasa imekuwa ni tatizo wananchi hawapati maji.

Je, ni lini hasa wizara hii itafanya utafiti wa kina kuona kwamba wale wananchi waliokuwa wakipata maji sasa hayapatikani na watakuwa sasa wanayapata, na wale waliokuwa hawapati maji ili wapate maji na mwishowe kuondoa tatizo hilo na kukidhi azma ya serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe.Mwakilishi kwamba kuna baadhi ya wananchi walikuwa wanapata maji kipindi cha nyuma, lakini sasa hivi hawapati maji, lakini suala hili nafikiri nimelijibu katika swali mama, kwamba kiwango cha maji kimepungua duniani. Kwa hivyo, hili suala linajulikana na tunazidi kufanya utafiti ili kuliondoa tatizo hili. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni inatakiwa tutoe majibu ya maswali ambayo ni ya uhakika. Pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini jana nimepata malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi wa Kijitoupele Shehia ya Changawe, kuwa kuanzia juzi wamekatiwa maji moja kwa moja, hawapati tena eneo kubwa shehia nzima. Je, hili linahusiana na kupungua kwa maji huko duniani. (*Kicheko)*

Mhe. Spika: Sasa hii ni kuhusu utaratibu au ni swali jengine la nyongeza?

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ni utaratibu.

Mhe. Hija Hassan Hija (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:

Skuli ya Sekondari ya Kengeja iko katika hali mbaya ya uchakavu na inatishia usalama wa wanafunzi wanaopata elimu katika skuli hiyo.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo ili kuepusha maafa katika skuli hiyo.

(b) Katika mwaka wa fedha uliopita serikali imetenga kiasi gani cha fedha ili kukarabati skuli hiyo ambayo kwa sasa kuta zake ziko kwenye hatari ya kubomoka, na bati zake zinavuja kwa uchakavu unaotokana na muda mrefu kupita tangu kujengwa kwa skuli hiyo mwaka 1926.

(c) Kwa kuzingatia kwamba walimu wanaishi mbali na eneo la skuli hiyo. Je, serikali ina mpango gani kuwapatia huduma ya usafiri ili kuondoa tatizo la usafiri kwa walimu na wanafunzi, hasa inapotokea dharura ya ugonjwa kwa mmoja wao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake namb. 5 lenye a, b, na c. Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Skuli ya Sekondari ya Kengeja ni moja kati ya skuli za zamani ambayo imeanzishwa mwaka 1926.Skuli hiyo ina majengo matano yenye madarasa 12, pia lipo jengo moja jipya lenye madarasa matatu ambalo limefikia hatua ya kuezekwa. Baadhi ya majengo yake ya zamani yalijengwa kwa kuta za mabati na hivi sasa yamechakaa baada ya kutumika kwa muda mrefu.

Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 wizara ilivunja jengo moja lenye madarasa mawili na kulijenga upya na hivi sasa linatumika. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Wizara itaendelea na juhudi za kufanyia matengenezo majengo ya skuli hiyo hatua kwa hatua, kutegemea na uwezo wetu wa kifedha. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 wizara ilitenga jumla ya shilingi milioni 20 kwa kukamilisha ujenzi wa jengo moja la skuli ya Kengeja Sekondari. Hivi sasa kazi ya kukamilisha ujenzi wa jengo hilo la madarasa matatu zinaendelea, kazi ya uezekaji, upigaji plasta na sakafu zimekamilika na kazi zilizobaki ni upakaji wa rangi na *apron* kwa nje. Hata hivyo jengo hilo hivi sasa linatumika na hapa Mhe. Spika, naomba kutoa wito kwa wananchi wa Kengeja kushirikiana na wizara katika kufanyia matengenezo majengo yaliyobaki. Kwa ushirikiano wetu ndio tunaweza kukamilisha majengo yote ya skuli zetu.

(b) Katika mwaka wa fedha 2010/2011, jumla ya shilingi milioni 10 zilitumika kwa matengenezo ya jengo moja la skuli hiyo.

(c) Wizara haina utaratibu wa kutoa huduma ya usafiri kwa walimu wa skuli za msingi na sekondari isipokuwa kwa skuli zenye dakhalia tu. Hata hivyo, kwa walimu wanaoishi mbali sana na skuli wanazosomesha, walimu wanalipwa nauli kila mwezi kwa mujibu wa nauli za serikali zilivyopangwa. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Spika nami kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe.Spika, katika Skuli ya Kengeja kuna majengo ya skuli ya msingi, kwa muda mrefu majengo yale bado hayajamalizwa. Je, wizara haioni kwamba ipo haja ya kuyamaliza majengo yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli Skuli ya Kengeja Msingi ina majengo ambayo wameanzisha madarasa saba, nilipokwenda ziara niliyaona majengo hayo na Kamati ya Wazee iliopo pale pamoja na walimu, wakatwambia kwa sababu majengo yale ni ya muda mrefu, na majengo yale tuliyatia katika Mradi wa *SIDA*, lakini wenzetu hao kidogo wamechelewa kutusaidia. Kwa hivyo, wizara imeyachukua majengo yale na tayari hivi sasa tumeanza kazi ya uezekaji na kazi nyengine zitafuata kadiri ya hali ya fedha itakavyoruhusu katika wizara.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe.Naibu Waziri katika jibu lake mama kasema kuna banda moja la vyumba viwili liliangushwa na limejengwa na sasa linatumika. Nataka Mhe. Naibu Waziri aniambie hilo ni banda gani lililovunjwa likajengwa na kuanza kutumika.

Mhe.Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, katika jibu langu mama nilisema skuli ile ina majengo matano na katika majengo hayo kuna jengo ambalo lina vyumba viwili, kwa mwaka wa bajeti wa 2010/2011 tulilivunja na tumelijenga na tayari linatumika. Kwa hivyo, Mheshimiwa ni Mwakilishi wa Jimbo hilo lakini nadhani hapiti. Mimi binafsi mwezi uliopita nilikuwa na ziara na nikakuta jengo hilo tayari wanafunzi wanalitumia na kwa hili ambalo lina madarasa matatu na nimesema kuwa, liko katika hatua ya mwisho ya utiaji rangi, pia wanafunzi wamo wanasoma. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe.Spika: Nyanyuka basi Mheshimiwa kama unataka kusema utaratibu.

Mhe.Mohammed Haji Khalid: Mimi ni kweli Mwakilishi wa Jimbo la Mtambile na natoka Kengeja, nililosema sikusema kwa kubahatisha, hakuna jengo lililoangushwa na wizara ikalijenga. Ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe.Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nisaidie ili tafsiri ya watu wawili ikae sawa kwa faida ya Baraza. Mhe. Spika, kamati yangu ya Baraza la Wawakilishi nikiwa Makamo Mwenyekiti nilifika Kengeja, jengo ambalo Mhe. Waziri anazungumza ni jengo ambalo ni jipya limeanzishwa *fresh*, hilo ni jipya, lakini jengo ambalo limeanguka mpaka leo hii halijajengwa. Kwa hivyo, maneno ya Mwakilishi ni sahihi.

Mhe. Salim Nassor Juma: Mhe. Spika, kanuni ya 58(3) Mhe. Spika, kinasema kwamba, "Mambo yanayofaa na yasiyofaa kuzungumzwa ndani ya hichi chombo, Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo yake ni sahihi…" naomba nimalizie hapo.

Sasa naomba Mhe. Spika, kwamba Mhe. Naibu Waziri kasema kuwa Mhe. Mwakilishi wa jimbo lile hapiti, kwa vile atupe ushahidi kuwa hapiti, ana ushahidi gani uliomfanya aseme kuwa hapiti, ikiwa hana ushahidi bora afute maneno yake kusudi tumsafishe huyu Mheshimiwa katika chombo hiki adhimu.

Mhe.Spika: Kilichompelekea Mhe. Naibu Waziri aseme kwamba Mwakilishi anafikiria labda hapiti ni kwamba shughuli zinazofanywa pale yeye inaonekana hazijui. Nafikiri hajakusudia hasa kwamba hapiti katika jimbo, yeye mwenyewe anakaa ndani ya jimbo bila shaka. Sasa kupita ni kufuatilia zile shughuli zenyewe zinazohusu, sio kwamba hapiti labda anakaa Unguja na jimbo liko Pemba, sifikirii kama amekusudia hivyo. Lakini kwamba katika zile shughuli ambazo zinafanyika ndani ya jimbo yeye hakuwahi kushuhudia akaziona, ndicho nadhani alichokikusudia Mhe. Naibu Waziri, lakini kwamba hapiti ndani ya jimbo nadhani si kweli, kwa sababu mwenyewe anakaa humo humo ndani ya jimbo.

Sasa kidogo nadhani hapa pana tatizo, labda mimi niseme kwamba ni namna tunavyotafsiri hili neno kuwa hapiti, labda kuwa yeye anakaa Bububu kwa mfano lakini jimbo liko kule Mtambile Pemba na Kengeja ikiwa ni eneo la jimbo lake. Nakusudia ni kwamba yale yanayotendeka mle shughuli za kila siku kuna nyengine hakuwahi kuzishuhudia, nadhani ndicho kinachokusudiwa. Sasa labda hili lisituletee mjadala wa kuona kuwa Mwakilishi huyu amelikimbia, hajakimbia jimbo, yeye anakaa humo humo, na ni mmoja kati ya wawakilishi wangu ambao mara tukifunga Baraza, wala simuoni hapa Unguja wengine huwa nawaona.

Kwa hivyo, mimi nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza kwamba huwa simuoni ndani ya eneo hili wakati hapana kazi, bila shaka anakuwa jimboni kwake, sijasikia wala hajaniaga kwamba anakwenda Dar es Salaam au kwengineko. Nadhani tumalizie hapo na nichukue nafasi hii vile vile kushukuru kwa kazi nzuri inazofanya wizara ili kuona mambo yote yanakwenda vizuri katika wizara hii na katika jimbo hili, na maeneo mengine ambayo shughuli zinafanyika. Mhe.Naibu Waziri nakushukuru na Mhe. Mohammed Haji Khalid nakushukuru sana kwa kazi zako nzuri.

Nam. 77

Vituo vya Kununulia Karafuu

Mhe.Salim Abdulla Hamad - Aliuliza:-

Kabla ya serikali kupandisha bei ya karafuu, Shirika la Biashara la Taifa *(ZSTC)* lilikwishavivunja vituo vingi sana vya kununulia karafuu, jambo ambalo lilisababisha wizara hii kujenga vituo vipya.

a) Wizara imejifunza nini kutokana na hali ya nyuma ilivyokuwa na baada ya wizara kujenga tena vituo vilivyovunjwa.
b) Ununuzi wa karafuu katika vituo vipya na vya muda ulikuwaje.
c) Wizara imejipanga vipi kwa kuongeza vituo vya kununulia karafuu kwa sehemu ambazo kumekuwa na vituo vya muda.

Mhe.Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Ahsante sana Mhe.Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mheshimiwa Mjumbe swali lake Nam. 77 lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, naomba nianze kwa kutofautiana naye Mhe. Mwakilishi kwamba, kuna vituo vya ununuzi wa karafuu vilivyovunjwa na serikali katika msimu wa karafuu uliopita. Ila ukweli ni kwamba kulikuwa na baadhi ya vituo, kama vituo vya Mtambwe, Donge na Micheweni ambavyo vilikuwa havitumiwi kununulia karafuu, na hii Mhe. Spika, ilikuwa ni kutokana na sababu zifuatazo:-

i) Idadi ndogo ya karafuu iliyokuwa ikipelekwa vituoni humo wakati huo
ii) Kushamiri kwa magendo ya karafuu na kuifanya *ZSTC* kushindwa kununua karafuu wakati huo.
iii) Na wakati mwengine Mhe. Spika, wafanyakazi wa *ZSTC* pia walipokuwa wakijaribu kwenda kununua karafuu walikuwa wakifukuzwa.

Mhe.Spika, ni zoezi la kawaida kwa nyakati za msimu wa karafuu *ZSTC* kununua karafuu kwa utaratibu wa kuanzisha vituo vya muda, kwa njia ya kutumia pengine gari kwa ajili hiyo.

Mhe.Spika, katika msimu huu baada ya kutangazwa kwa bei mpya ya karafuu, na jinsi wananchi walivyojitokeza kuiunga mkono serikali yao kwa kuuza karafuu zao katika vituo vya *ZSTC*, serikali iliongeza vituo vipya sita kutoka vituo 32 vilivyokuwepo awali kutokana na kuongezeka kwa wingi wa karafuu zilizokuwa zikipelekwa vituoni.

b) Mhe. Spika, kwa jumla ununuzi wa karafuu katika vituo vipya na vya zamani ulikuwa mzuri na wa kutia moyo sana, kwani wananchi walionesha ushirikiano, kama nilivyosema kwa serikali yao kwa kuliokoa zao la karafuu, ambalo ndio tegemeo la uchumi wetu. Hali hii inatokana na kupita kwa lengo la ununuzi wa karafuu ambapo serikali kama tulivyotangaza juzi, iliweza kununua jumla ya tani 4,726 kutoka tani 3,000 zilizokadiriwa na serikali. Kiasi hicho Mhe. Spika, ni kuvuka kwa lengo kwa zaidi ya asilimia 50.

c) Mhe. Spika, serikali kupitia mkakati wa kuendeleza soko la karafuu na mpango mageuzi wa *ZSTC*, utavifanyia matengenezo vituo vya zamani vya kununulia karafuu, kwa kujenga sehemu maalumu ya ulipaji fedha, na sehemu ya manunuzi, pamoja na kuweka huduma ya vyoo, maji, viti, meza na mabenchi ya kukalia kwa wauzaji wa karafuu. Pia serikali itaendelea kujenga vituo vipya, kwa kadiri mahitaji yatakavyojitokeza, kwa kuzingatia wingi wa karafuu zitakazokuwa zinapelekwa katika maeneo husika.

Mhe.SAlim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata kuuliza swali la nyongeza. Mhe.Spika, pamoja na kuwa Mhe. Waziri katika kujibu swali langu hakukubaliana na mimi kuwa kabla ya serikali kupandisha bei ya karafuu, Shirika hili la Biashara la Taifa (*ZSTC*) lilikwishavunja vituo vingi. Hii ndio hali ilivyo na ndio sababu nikaleta hili swali na katika baadhi ya vituo vilivyovunjwa ni kituo cha Mtambwe Kaskazini ambacho naamini safari hii baada ya kujengwa tena upya kwa makelele niliyokuwa nikiyapiga humu limenunua karafuu nyingi sana.

Pili Mhe.Spika, swali (c) Mhe.Naibu Waziri hakulijibu ipasavyo.Kwa sababu Mhe. Spika, nimeshuhudia vituo vingi kuwa vilivunjwa na vyengine ikabidi kwenda wenyewe *ZSTC* kuomba kuwa visivunjwe. Swali hilo lilikuwa

limeulizwa kuwa wizara imejipanga vipi kwa kuongeza vituo vya kununua karafuu kwa sehemu ambazo kumekuwa na vituo vya muda.

Yaani safari hii kwa vile karafuu wamenunua kwa wingi kumeongezeka vituo vya muda, hata mimi katika jimbo langu nilikuwa na vituo viwili vya muda. Sasa kwa sababu pia viliuza karafuu nyingi sana, wizara kwa kunusuru hili zao la karafuu imejipanga vipi kuvijenga hata vile vituo vya muda ili wananchi watokane na usumbufu wa kuuza karafuu zao, ambapo kutopata nafasi ya kutosha ya kuuza karafuu, husababisha karafuu kusafirishwa kwa magendo.

Mhe.Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe.Spika, bado naendelea kusema kwamba serikali haikuvunja vituo vya kuuzia karafuu. Tutakumbuka Mhe. Spika, huko nyuma tunakotoka sio sasa hivi, ni wananchi na ni kutokana na jazba za kisiasa zilizokuwepo wakati huo ndio waliokuwa wakiviharibu vituo, na walikuwa hawapeleki karafuu vituoni na tunamshukuru Mwenyezi Mungu huko tumetoka, sasa sote tuko katika mstari mmoja tunaelekea kwenye kuijenga nchi yetu.Vituo Mhe. Spika, vinaimarishwa na tumeliona hili katika msimu huu wa karafuu.

Lakini kuhusiana na jibu (c) Mhe. Spika, nimejibu swali lake na naomba nirejee kwa maslahi yake yeye Mhe. Salim inaonesha hakusikia. Nimesema Mhe. Spika, nina-*quote*. "Aidha, serikali itaendelea kujenga vituo vipya kwa kadri mahitaji yatavyojitokeza, kwa kuzingatia wingi wa karafuu zitakazokuwepo katika maeneo husika". Nimeseme hilo Mhe.Spika.

Mhe.Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika kunipa fursa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Mhe.Spika, kwanza naishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara hii ya Biashara,Viwanda na Masoko kwa kuongeza bei ya karafuu na wananchi wetu wakafaidika. Wananchi wa Zanzibar wamefaidika sana na bei hii ya karafuu na pia wananchi wameitikia wito wa kuwataka waache kuuza karafuu kwa magendo, na badala yake kuiuzia serikali yetu ili kuleta faida katika nchi yetu.

Sasa namuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu wananchi wameitikia wito huo, na kununua karafuu hazipatikani mpaka mikarafuu yenyewe iwe ipo. Je, imejipanga vipi wizara yake kuwahamasisha wananchi katika upandaji wa mikarafuu mipya ili kuleta faida katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwanza nipokee pongezi alizozitoa kwa serikali, kufuatia hatua hii iliyochukuliwa na serikali katika suala zima la karafuu. Hivi ndivyo inavyotakiwa Mhe. Spika, pale ambapooserikali inastahili kupongezwa basi ipongezwe.

Mhe.Spika, katika kuhamasisha wananchi, serikali imeliona hilo kuhusu kuongeza uzalishaji wa zao la karafuu, na ndio maana tumesema kwamba Shirika la *ZSTC* linafanyiwa marekebisho kwa lugha ya kigeni *restructuring*, tukiwa tumezingatia kwamba, kwa kushirikiana na wizara husika, Wizara ya Kilimo na Maliasili suala zima la kuotesha miche mipya ya karafuu kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa karafuu, nalo litazingatiwa baada ya kulifanyia marekebisho makubwa Shirika hili la *ZSTC*.

Mhe.Spika, lakini pia kutakuwa na mfuko maalumu wa kuendeleza zao la karafuu ambalo nalo hili kama Mhe.Mwakilishi alisikiliza hotuba ya Mhe. Waziri juzi, wakati tunazungumza na wananchi kuhusu azma ya serikali kupitia wizara yetu kufunga msimu huu wa karafuu. Hili Mhe. Waziri alilieleza vizuri sana kwamba kutakuwa na mfuko wa kuendeleza zao la karafuu, na itazingatia suala zima la upandaji mikarafuu mipya.

Nam. 8

Upungufu wa Wafanyakazi wa "*Orderly*" Mnazi Mmoja

Mhe.Salim Abdalla Hamad (Kny.Mhe.Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Wafanyakazi katika kada ya *orderly* ni wachache sana kiasi cha kufanya huduma ya wagonjwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe ni ya kuzorota mno.

(a) Ni kwa kiwango gani Serikali inalielewa hili.

(b) Ni vipi Serikali inapanga angalau kupunguza makali ya tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 8 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba nianze kutoa maelezo kidogo kuhusu hili suala. Tunazungumzia *orderly, orderly* kwa utaratibu ni neno la Kiingereza lakini linalohusiana na mambo ya afya linalosema neno kwamba ni msaidizi au kwa neno la Kiingereza linaitwa *helper*.
Sasa *orderly* si katika kada za afya bali ni wasaidizi wa usafi katika hospitali na vituo vya afya. Kwa hiyo, ni wasafishaji kama wanavyosafisha katika ofisi nyengine lakini hawa wanasafisha katika mahospitali na vituo vya afya.

Tunapozungumza wataalam tunasema kwamba kada za afya zinahusisha wale wataalam wanaosomea mambo ya afya, madaktari na wengineo tunaowafahamu.

Baada ya maelezo hayo, napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake.

a) Serikali kwa kiwango cha uhakika tunajua upungufu tulionao kwa wafanyakazi wa aina zote ikiwemo hao ma-*orderly*.

b) Serikali inatoa nafasi kadhaa za ajira kwa kila wizara na kila aina ya wafanyakazi pale inapokuwa na uwezo wa kuwaajiri. Ni ukweli usiofichika kwamba mahitaji yetu ya *orderly* na kada nyenginezo Wizara ya Afya ni makubwa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kupata taaluma ya kisayansi kutoka kwa Mhe. Waziri kuhusu neno *orderly*. Lakini nashukuru kwa kukiri kuwa kuna upungufu mkubwa wa watendaji wa kada mbali mbali katika wizara hii. Kwa vile Mhe. Spika, naelewa kuwa Chuo cha Afya Mbweni kimetoa vijana wazuri tu wa kuweza kusaidia kufanya kazi japokuwa si ya kitaalam katika kada hii ya afya.

Je, Mhe. Waziri, ana mpango gani wa kuanza kuajiri wafanyakazi hasa katika zile sehemu zenye matatizo makubwa kuliko nyengine na hasa ikiwa ni katika vijiji.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba Chuo cha Afya Mbweni kinatoa wataalam wa kada tofauti zile ambazo zinaweza zikasomeshwa katika chuo chetu. Pale ambapo wataalam wanatoka huwa tunawagawa kwa mujibu wa mapungufu. Si Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tu inayopitia skuli zake na Wizara ya Afya utaratibu ndio huo huo. Nimepitia vituo vyote vya Unguja na Pemba kwa asilimia mia moja na ninajua wapi kuna upungufu na ninapowapata ninawapanga kwa utaratibu wa mapungufu. Ndio maana mwaka jana Pemba ilipata asilimia 60 ya wafanyakazi na waliobakia ndio wakabaki Unguja. Kwa hiyo, tunajua tunachokifanya.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa rasilimali watu tena wenye afya ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Kwa kuwa *orderly* ni wafanyakazi muhimu sana sio tu kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa lakini hata katika kuwasaidia wauguzi pamoja na madaktari. Kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri kwamba kuna upungufu wa wafanyakazi wakiwemo ma-*orderly*.

Je, serikali kuendelea kutoajiri ma-*orderly* si kudharau rasilimali watu wa nchi yetu na kutoa kazi ngumu kwa madaktari pamoja na hawa wauguzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, mimi nafikiri tunapozungumza suala la rasilimali watu sio binaadam tunazungumzia utaalam wa watu. *Orderly* hana utaalam, rasilimali watu ya Wizara ya Afya ni madaktari mpaka kufikia msaidizi mkunga. Kama ni suala la watu tu kuwajaza sehemu hilo ni jengine, lakini hata hivyo nimesema kwamba serikali nayo ina uwezo wake maalum. Ikitupa kwamba tunaajiri ajirini ma-*orderly* 10 tutaajiri 10 kwa sababu ndio uwezo wake.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa hivi sasa ma-*orderly* wote wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ni wataalam sawa sawa na manesi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwangu mimi kama mtaalam ni yule anayesoma akapata cheti. Kufanya kazi kwa kuibia kazi za wengine hilo halimhalalishi *orderly* kuwa ni mtaalam.

Nam. 33

Ujenzi wa Matuta kwa Barabara zilizokuwa karibu na Skuli

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza**:**

Mhe. Waziri nilipokuwa nikichangia kwenye Bajeti ya Wizara yako nilizungumzia suala la kujenga matuta kwenye sehemu za barabara ambazo ziko karibu na skuli, ili kuepusha ajali za mara kwa mara za wanafunzi wa skuli mbali mbali. Kwa mfano, Skuli ya Mtambile, Madungu, Michakaeni, Mbuzini, Minungwini na kadhalika.

Je, Mhe. Waziri, Wizara yako ina mpango gani wa kulishughulikia tatizo hilo ili kuwanusuru watoto wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 kama ifuatavyo:-
Tabia ya madereva ya kuendesha vyombo vya moto kwa mwendo wa kasi na kutokufuata sheria za barabarani kunachangia kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani. Tunaomba madereva kuwa waangalifu sana ili kuepusha ajali za barabarani ambazo nyingi zinatokana na uzembe.

Ujenzi wa matuta barabarani ni sehemu ya utunzaji wa barabara ambapo kiasi kikubwa cha fedha kinatoka katika Mfuko wa Barabara.

Wizara yangu ina mpango endelevu wa kuweka matuta katika maeneo maalum kwenye barabara zetu kama inavyoonekana katika sehemu mbali mbali Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, hivi sasa tumeomba fedha za kujenga matuta katika vijiji kadhaa, sehemu za masoko na skuli zikiwemo skuli za Mtambile, Mbuzini, Minungwini, Sokoni Kianga, Sokoni Mapofu, Kiuyu na kadhalika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sehemu nyingi tunazoziona kwenye barabara zetu ambazo zinajengwa matuta na hakuna aina moja ya matuta.

(a) Je, Mhe. Waziri matuta haya yanajengwa kila mtu na vyake au kuna kipimo maalum.
(b) Ni nani hasa mhusika wa kujenga matuta hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, matuta ya barabarani yako ya namna kadhaa na vipimo mbali mbali inategemea aina ya barabara unayojenga matuta. Kwa hivyo, kuna viwango maalum kufuatana na aina ya barabara ilivyo. Wajenzi wa matuta haya ni serikali kwa kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na kwa kutumia Idara yake ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, suala la matuta katika kupunguza ajali ni suala muhimu sana, lakini na *roundabout* ni sehemu moja ya kupunguza ajali katika nchi yetu. Sasa tuliona wataalam wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wakipima katika kujenga *roundabout* ya Mwanakwerekwe ili kupunguza ajali za barabarani. Lakini *roundabout* ile imejengwa ambapo haikidhi haja na sasa hivi tayari imeshabomoka.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotumika katika kujenga *roundabout* ile.
(b) Je, Wizara yake itakuwa tayari kujenga *roundabout* nyengine ili kupunguza ajali katika barabara zetu za Zanzíbar.

Mhe. Spika: *Roundabout* na matuta. Hebu tafuta utaratibu wa kuuliza swali la msingi.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kama alivyoeleza mwenyewe Mhe. Waziri kwamba matuta yako ya aina nyingi bahatí mbaya hakuyataja nikayajua. Lakini kuna matuta mengine yamekaa kama minazi iliyonyooshwa barabarani. Mhe. Spika, nitoe mfano hii barabara inayotoka hapa Chukwani kwenda Mazizini.

(a) Je, Wizara imefanya utafiti gani kuona matuta yale hayana athari kwanza kwa gari.
(b) Je, wamefanya utafiti gani kuona kwamba matuta yale yanazuia gari kwenda kwa kasi. Maana yake huona yale matuta yanaumiza gari halafu watu wanayachupa kwa kasi zao zote.
(c) Je. Mhe. Waziri haoni haja ya kuyabadilisha haya matuta akaweka mengine yale mapana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi amezungumzia barabara ya Chukwani hii ni barabara inayotoka Polisi Mazizini mpaka Chukwani Jeshini. Matuta anayoyazungumzia ni matuta ambayo yameanza Kiwanda cha Matrekta mpaka mwisho wa barabara ambapo daladala zinaishia. Nakubali kabisa kwamba matuta yale hayana *uniformity* na yamejengwa katika utaratibu ambao maderera na hasa abiria wamekuwa wakilalamika. Baada ya kugundua utaratibu huo tumeomba fedha kujenga matuta ya kisasa kwa barabara ile pamoja na Bububu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ni kweli kabisa kwamba matuta yale ambayo yamejengwa yanakera na kwa kuona hilo tumeona bora tuyabadilishe na tuweke matuta ambayo ni *standard*.

Nam. 141

Ucheleweshaji wa Vyeti vya Kuzaliwa

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza**:**

Kwa muda mrefu sasa wananchi wa Zanzibar wamekuwa wakilalamika juu ya urasimu uliopo katika Afisi ya Mrajis wa Serikali kutokana na vyeti vya kuzaliwa hasa kwa watoto wadogo kuchelewa. Mara nyengine huchukua muda mrefu na usumbufu mkubwa hadi kupatikana kwake.

(a) Je, Mhe. Waziri, kuna sababu gani zinazopelekea hali hiyo.

(b) Je, huoni kwamba hali hii huwakatisha tamaa wananchi wetu na kuwafanya waamini kwamba Serikali yao haiwatumikii.

(c) Ni hatua gani utakazochukua kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 141 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kabisa kwamba vyeti vya kuzaliwa mara nyengine huchukua muda mrefu kupatikana. Wizara yangu inakerwa sana na usumbufu unaowapata wananchi wetu katika suala hili. Mhe. Spika, suala hili mimi binafsi, Wizara yangu na Serikali kwa ujumla linatukera na tunajitahidi kulitafutia ufumbuzi na zaidi ni kwamba hatulipendi hata kidogo kutokea.

Mhe. Spika, Wizara yangu katika juhudi zake za kulitatua tatizo hili imefanya utafiti wa kina kama ifuatavyo na kuona kwamba:-

i. Kwa Mkoa wa Mjini Magharibi kuna vyeti 3,813 ambavyo wenyewe wameshalipa lakini bado hawajavipata.
ii. Wilaya ya Kaskazini A ni 2,145
iii. Kaskazini B ni 40
iv. Micheweni 500
v. Mkoani 1,700
vi. Wete 502 na
vii. Chake Chake 1,506
Jumla 10,206

Mhe. Spika, sababu kubwa za mrundikano huo ni pamoja na:-

(a) Kutokupatikana vyeti vya kutosha kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

(b) Kuwatumia Maafisa wa Wilaya kwa kazi za usajili, ambapo Afisi yetu huwa haina uhusiano nao wa moja kwa moja. Maafisa hawa hudiriki kuchukua likizo ama la kawaida au la uzazi bila ya Afisi ya Mrajis Mkuu kujua na hivyo kusitisha zoezi zima la utoaji vyeti katika Wilaya husika.

(c) Uhaba wa wafanyakazi wa kutoa huduma za utoaji vyeti katika Afisi za Wilaya na ya Mrajis.

(d) Kutokuwa na fedha za kutosha za kununulia vyeti na wakati tunapozipata bei za vyeti huwa zimepanda na hivyo kuzidi kupunguza idadi ya vyeti tunavyovihitajia.

Mhe. Spika, licha ya vikwazo hivyo tumeshachukua hatua kadhaa za kupunguza matatizo hayo:-

(a) Mhe. Rais ameteua Mrajis na Naibu Mrajis wa Vizazi na Vifo ambapo sasa kazi za usajili zimerahisika.

(b) Kuukata kabisa urasimu kwa kuwahamisha baadhi ya watendaji wetu waliopo katika ofisi zetu ambao tulihisi wanaleta urasimu usio na maana.

(c) Kuwalipa wafanyakazi *overtime* ili vyeti vyote kwa Mkoa wa Mjini Magharibi viwe tayari ifikapo tarehe 31/03/2012. Mhe. Spika, ninafuraha kusema kuwa kazi hii sasa imefikia asilimia 90 (90%) na tunawahakikishia wananchi wote wa Wilaya ya Mjini na Magharibi kwamba hivi sasa wananchi wengi wameshaanza kuchukua vyeti vyao.

Mhe. Spika, tunahakikisha vile vile kwamba ifikapo tarehe 31 Machi, 2012 vile vyeti ambavyo tumevisema kwa Mjini Magharibi vitakuwa vyote tayari vimeshapatikana.

(d) Tumejitahidi kutafuta pesa na kufanikiwa kupata vyeti kiasi 15,000 ambazo zitatosheleza kwa kupiga chapa vyeti vyote tunavyodaiwa na kazi hii imeshaanza.

(e) Kuweka utaratibu maalum wa vile vyeti vya Wilaya zilizobaki viletwe Afisi ya Mrajis ili wapiga chapa wetu waifanye kazi hiyo haraka haraka kama iwezekanavyo na pia tutawapa *overtime* ili waweze kukamilisha vyeti hivyo kama tulivyofanya kwa Mjini Magharibi.

(f) Mhe. Spika, mpango kama huo tutauendeleza Pemba baada ya kumaliza Unguja.

Mhe. Spika, ninaaminji kwa mpango huu tuliouanza, basi ifikapo mwezi April mwisho suala hili *inshaallah* litakuwa halipo tena au kubakia kidogo sana ambapo haitazidi mwezi Mei itakuwa tatizo hili limeondoka kabisa.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ninaamini wananchi wetu hawatakata
tamaa, bali watakuwa ni mashahidi wa nini Serikali yao inafanya kwa
kuwaondolea shida wananchi wao. Haya yatathibitishwa zaidi na wananchi wa Wilaya ya Mjini na ya Magharibi kwani kufikia hii leo asilimia kubwa sana wananchi hao wameshapata vyeti vyao.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wakati alipokuwa akijibu alisema suala moja linalosababisha usumbufu wa kupatikana vyeti kwa wakati ni tatizo la fedha. Lakini mimi ninavyofahamu kwamba wananchi vile vyeti hawapewi bure hulipia zile fedha zinakwenda wapi.

La pili kuhusu usumbufu unaojitokeza mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri. Je, atakubaliana na mimi kwamba kuhamisha ile ofisi kutoka jengo la Mambo Msiige ambako walikuwa wakifanya kazi kwa nafasi kuipeleka pale kwenye jengo la *PBZ* kumechangia usumbufu huo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ni kweli kwamba vyeti vinauzwa lakini napenda ajue tu kwamba zile ni pesa za serikali, unapouza sisi tunapopata fedha lazima tuzipeleke Hazina na Hazina wanagawa fedha kwa mujibu wa utaratibu waliouweka. Sasa unajua matatizo ambayo yanaweza yakatupata Hazina unaweza ukaomba fedha zikachelewa. Kwa hivyo, si kwamba vyeti vile tunauza na fedha tunakuwa nazo sisi.

Mhe. Spika, suala hili kwa kuona hayo tumeshazungumza serikalini na tumepeleka ombi letu makusudi la kupunguza matatizo haya na ninaamini serikali imeliona na tumeahidiwa kwamba kuanzia mwaka wa fedha unaofuata tutapata *retention* ambayo itasaidia sana kupunguza matatizo haya.
Suala la pili sikubaliani nae kwamba jengo lile la Mambo Msiige ndilo linalofanya upungufu au matatizo haya. Kwa sababu vyeti vyote hivi sasa vinatolewa katika Wilaya, Wilaya ya Kaskazini, Wilaya ya Kusini, Wilaya ya Kati na Wilaya ya Mjini Magharibi. Sasa pale ni *headquarter* tu tunasimamia utoaji wa vyeti.

Sasa matatizo mengi yako katika Wilaya kama nilivyosema mwanzo na tumeshagundua hasa Wilaya ya Kaskazini 'A' mfanyakazi alichukua likizo la miezi mitano ambaye ndie aliyekuwa akipiga vyeti. Kwa hivyo, utoaji wa vyeti ulisimama pale kwa kiasi cha miezi mitano na sisi tulikuwa hatuna habari. Baada ya kugundua hivyo ndio tukafanya hatua za haraka kuchukua vyeti vile na kuweza kuvipiga katika afisi kuu.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wakati anajibu swali mama la upatikanaji wa vyeti hivi ambavyo ni tatizo sugu mno alitaja Wilaya za Unguja pekee kwamba matarajio mwezi wa nne *inshaallah* mambo yatakuwa mazuri. Je, kwa zile Wilaya za Pemba ambapo Wilaya ya Wete imekithiri kuliko nyengine zote 10 anatwambia nini.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza sikubaliani nae kwamba Wilaya ya Wete imekithiri. Wilaya ya Wete ina vyeti 502 vilivyokuwa havijatolewa, Wilaya ya Chake Chake ina vyeti 1,500, Wilaya ya Mkoani 1,700 na Wilaya ya Micheweni 500 kwa hivyo Wilaya ya Wete haikukithiri iliyokithiri ni Wilaya ya Chake Chake na Mkoani.

Lakini la pili nilisema Mhe. Spika, kwamba hizi hatua za dharura tumezianza kwa hapa Unguja na katika jibu mama nilisema kwamba tunapomaliza basi tutakwenda Pemba. Tumefanya hivi kwa makusudi kwa sababu tunawatumia wafanyakazi wetu waliopo afisi kuu, wale ndio wana ujuzi mkubwa kwa sababu kule kwengine aliyeko ni mtu mmoja mmoja tu.

Sasa tukishamaliza kutatua yote hapa wale tutawapeleka Pemba watasaidiana na wenzao na shughuli hii itamalizika. Kwa sababu wanakwenda kama ni *task force* ninaamini katika kipindi kifupi sana shughuli hii itamalizika. Siwezi kutoa uhakika hapa lakini ninaamini kwamba kabla ya Bajeti tukijaaliwa basi suala hili linaweza likamalizika moja kwa moja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tumebakiwa na maswali matatu yaliyoletwa katika *order paper* ya leo na ninazo taarifa kwamba shughuli inayofuata huenda isiende kama vile ilivyokusudiwa taarifa atakuja kutoa mwenyewe Mhe. Mwanasheria Mkuu baadae. Lakini angalau kwa leo maswali haya tuyamalize nadhani mtakubaliana nami kwa kumuomba Mhe. Waziri atoe hoja ya kuendelea na maswali haya yaliyobaki matatu na baada ya hapo tena tuendelee na shughuli iliyopo ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu atatoa taarifa juu ya hilo jambo ambalo lipo mbele yetu baadae.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa kipindi cha maswali kimemalizika na kwa kuwa bado muda tunao wa kuweza kumaliza maswali yaliyo mbele yetu, naliomba Baraza lako tukufu liweke kando kanuni ya muda wa maswali ili tuweze kumalizia maswali matatu yaliyo mbele yetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nam. 53

Nyongeza ya Mishahara kwa Wahasibu

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Serikali imeamua kupandisha maslahi ya wafanyakazi wote wakiwemo wataalamu wa kada mbali mbali. Miongoni mwa wataalamu waliozingatiwa ni pamoja na Wahasibu. Lakini zipo taarifa kua kuna tofauti ya malipo kati ya Wahasibu wa Unguja na wale wa Pemba.

(a) Nini ukweli wa suala hili.

(b) Iwapo Wahasibu wa Makao Makuu ya Mawizara wanapewa maslahi zaidi kuliko wenzao wa Pemba na maeneo mengine ya Maidara pamoja na kua na sifa zinazolingana za kielimu, uzoefu na kadhalika. Je, huo si ubaguzi wa makusudi.

(c) Je, ni nani anaependekeza maslahi ya Wahasibu Unguja na ni nani anaependekeza maslahi hayo Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Si kweli kwamba Wahasibu wa Unguja na Pemba wanalipwa tofauti ya mishahara.

(b) Wahasibu wenye elimu zinazolingana Unguja na Pemba wanalipwa mishahara ya aina moja, isipokua Mhasibu Mkuu wa Wizara na Mkaguzi Mkuu wa Wizara au Mhasibu anaesimamia fungu la matumizi anapata maslahi zaidi. Kwa mfumo wa kiutawala wa SMZ, tuna Mhasibu Mkuu mmoja kwa kila fungu la matumizi na mapato na kama ilivyo kwa Maafisa Wahasibu (*Accounting Officers*).

(c) Suala la malipo ya Wahasibu linasimamiwa na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambapo kigezo ni elimu na muda wa utumishi bila ya kuangalia kama yupo Unguja au Pemba.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri, nina swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Waziri alipokua akijibu swali langu la msingi la kwanza, alisema kwamba sio kweli kwamba Wahasibu wa Pemba na Unguja wanalipwa tofauti. Lakini wajumbe wako Mhe. Spika, wanapokwenda katika ziara za kamati basi Wahasibu wa Pemba wamekua wakitoa kilio hiki kwa muda mrefu kwa kupitia kamati mbali mbali.

Je, Mhe. Waziri sasa atakua tayari kufanya utafiti juu ya suala hili, kwa sababu taarifa ambazo zilizokuwepo kwenye Kamati ndio hizi zinazosema kwamba Wahasibu wa Pemba wanapewa mishahara tofauti na Wahasibu wa Unguja, pamoja na Wahasibu wa Idara na taasisi nyengine za Serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, napenda nisisitize majibu yangu kwamba hakuna tofauti ya kulipwa mishahara kati ya Wahasibu wa Unguja na Pemba. Kinachoendelea ni kwamba

kuna tofauti ya Mhasibu Mkuu wa Wizara na Mhasibu wa Ofisi Kuu Pemba. Mhasibu Mkuu wa Wizara au taasisi yoyote inasimamia fungu, huyu ni Mhasibu Mkuu na Mhasibu ambaye anasimamia vifungu vya taasisi au Ofisi Kuu Pemba anasimamia vifungu hasimamii fungu. Mhasibu Mkuu anasimamia fungu zima la Wizara, ikiwemo makao makuu pamoja na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, Mhe.Mjumbe ameniomba nifanye utafiti. Nataka nimuhakikishie kwamba kabla sijajibu swali hili nilifanya utafiti wa kutosha, ndio maana nikaja kujibu swali hili. Hata hivyo, napenda nimuhakikishie kwamba nitaendelea kufuatilia ili nijue kwamba hayo yaliyoonekana na kamati yana ukweli gani ili niweze kuchukua hatua.

Nam. 56

Vikosi vya SMZ

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Taifa lolote duniani hujivunia vikosi vyake vya ulinzi na usalama kwa hapa Zanzibar mbali ya kuwa na vikosi vya ulinzi vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia vipo vikosi vya SMZ ambavyo vinakabiliwa na changamoto mbali mbali, yakiwemo malalamiko ya askari wake.

(a) Zipo taarifa kuwa askari wa vikosi vya SMZ wamekua wakikatwa mishahara yao bila ya idhini yao. Je, hilo ni kweli.

(b) Je, suala la kuchangia michezo kwa Askari wa Vikosi vya SMZ ni la lazima au hiari.

(c) Ni hatua zipi zinazochukuliwa mpaka Askari wa Vikosi vya SMZ kupandishwa cheo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 56 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kiutaratibu hakuna mtumishi yoyote wa Serikali anaekatwa mshahara wake bila idhini yake, isipokua kama kumewekwa mpango wa kufanya hivyo.

Katika miaka ya nyuma idara maalumu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ziliweka utaratibu wa kukata posho la chakula kwa watumishi wake ambao wanaenda mafunzoni na wanaolala kambini. Huu ni utaratibu wa kawaida wa kiaskari.

Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kusitisha utaratibu huu baada ya kuona kwamba unazidisha mzigo kwa watumishi wa Idara Maalum. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hivi sasa imeagiza Idara Maalum zote kuhakikisha kuwa fedha hizo za kugharamia chakula zinaingizwa katika bajeti zao, ili askari waishio kambini wapatiwe chakula ipaswavyo bila kukatwa kwenye mishahara yao.

b) Mhe. Spika, katika kuimarisha michezo na afya Idara Maalum za SMZ zimeunda klabu mbali mbali za michezo na tunazipongeza, kama Chuo cha Mafunzo ndio bingwa wa *football* hapa Zanzibar. Wanachama wa klabu hizo ni watumishi wa Idara maalum wenyewe na hutoa michango ya hiyari kuziendeleza klabu zao. Nakiri hapo nyuma kulikua na michango kusaidia klabu hizo za michezo vikosini bila ya ridhaa ya wahusika wenyewe. Pia utaratibu huo tumeshaelekeza kwamba usitishwe.

c) Mhe. Spika, taratibu za kupandisha vyeo kwa maafisa na wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ hufanywa na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ baada ya kuangalia sifa na vigezo vya upandishaji wa vyeo, ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Waziri katika majibu yake ya msingi alisema kwamba suala la kukatwa mishahara

na kuchangia michezo, tayari wametoa maelekezo kwamba lisitishwe. Maelekezo ni suala jengine na hatua ni suala jengine. Je, Mhe. Waziri una uhakika kwamba hatua zinachukuliwa, kwa sababu sisi Wawakilishi, wako askari wetu wamekua wakilalamika kwamba bado wanaendelea kukatwa maslahi yao bila ridhaa. Sasa nilikua naomba nijue kwamba maelekezo uliyotoa yanafanyiwa kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kama nilivyosema nakiri kwamba hili suala lilikuwepo na tuliingilia kati kwamba lisitishwe mara moja. Tumefuatilia na tumegundua kweli kwamba kuna baadhi ya sehemu bado wanakatwa. Kwa hivyo, hilo tunalifuatilia, na sehemu tunayofuatilia sasa hivi ni Wizara kwa sababu hao ni *respective section* zile wenyewe tumeona bado wengine wanaendelea na huo utaratibu. Sasa tunafuatilia kiwizara wenyewe kuona kwamba hilo zoezi linasimamishwa, ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, wakati kamati yetu ya Katiba Sheria na Utawala tulipotembelea vikosi vya mafunzo, hasa kwa upande wa Pemba tuligundua kwamba katika changamoto nyingi ambazo tunakabiliana nazo ni pamoja na hali mbaya sana ya makaazi yao katika kambi mbali mbali kiasi ambacho hata haikidhi kukaliwa na binadamu wa kawaida, seuze kwa askari ambaye anawalinda wanafunzi katika vyuo vya mafunzo. Sijui Wizara inaliangalia vipi suala hili.

(b) Vile vile kumekua na changamoto nyengine kubwa sana ya askari hawa kutopatiwa maslahi yao hasa wanapopewa uhamisho. Sijui Wizara inalifuatilia kwa kiasi gani suala hili na kulipatia ufumbuzi, ili kuona hatua zinachukuliwa baada ya kuona ufuatiliaji ambao siku zote unakua hauna kikomo, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, sikulipata vizuri swali la kwanza, kwa sababu Mhe. Ismail Jussa anaelekea chini zaidi wakati akizungumza, kidogo sikulikamata. Lakini swali la pili naomba nilijibu kwamba ni kweli mimi mwenyewe nilifika Pemba nikakuta malalamiko ya baadhi ya maaskari ambao wamepewa uhamisho na hawakupewa tiketi ama posho lile la uhamisho. Kwa hivyo, nilifuatilia na nimeagiza wale ambao kweli wamejitegemea basi wa-*submit claim* zao na watarejeshewa pesa zao zote.

Pia tumeagiza kwamba kwa kweli idara lazima ijipange vizuri, ili wanapofanya uhamisho wa askari hawa basi kusiwe na usumbufu kama huu na wahamishwe ipaswavyo. Hilo swali la kwanza Mhe. Spika, ningeomba alirejee, sikulipata vizuri.

Mhe. Spika: Ni maeneo wanayokaa ambayo yako hali mbaya sana. Serikali imechukua hatua gani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, na swali hili nimshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kama alivyosema kwamba wametembelea na mimi mwenyewe nimetembelea na nakiri kwamba ni kweli, lakini tumeshachukua hatua na tumeshaanza kufanya ukarabati mkubwa sana. Mimi mwenyewe nilianza, nilikwenda Kangagani nikaona hali ilivyokua mwanzo, tukaelekeza na hali inaendelea vizuri. Juzi tu nilikua Wete pale nilitembelea zote, lakini kwa kweli kama hali yetu ya bajeti inavyoruhusu na sisi ndio tunavyokwenda. Lakini tumeona ni kweli kwamba hali sio nzuri hasa kwa upande wa Pemba, hilo tumeliona na tunalishughulikia ipaswavyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, alipokuwa Mhe. Waziri akijibu swali la nyongeza, alisema kwamba tayari alikwishakutoa agizo la askari kutokukatwa fedha zao za mishahara bila ridhaa na akasema kwamba tayari amekwishakutoa hilo agizo.

Mhe. Spika, mimi kamati yangu ndio inayosimamia Wizara ya Mhe. Waziri, mpaka tulipokwenda kwenye kamati bado askari wanaendelea kukatwa mishahara yao bila ya ridhaa yao. Swali langu liko hapa, je Mhe. Waziri kwa kuwa Wizara yako ndio inayosimamia vikosi vya SMZ na kawaida ya vikosi huwa wanakwenda kwa amri, sasa hii amri yako baada ya kuitoa kama haikuchukuliwa je, kuna hatua gani za kinidhamu zitachukuliwa kwa wale ambao wamekiuka agizo lako kama Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, baada ya Mhe. Hamza Hassan na timu yake, nakusudia timu yake ni kamati yake baada ya kuondoka Pemba tu, basi mimi nikapewa ripoti kamili waliyoyauliza, waliyoyafuatilia na hali waliyoiona na mimi nikafunga safari, kila walipopita wao na mimi nimepita nikaelezwa yote na nikawasilikiliza, yale waliyokuambia wewe na mimi wameniambia hayo hayo na niliwachukua makamanda wote. Niliporudi tu nikafanya kikao na makamanda wangu wote wa idara maalum, nikaagiza mara moja. Unajua na mimi ndio kamanda, sio kamanda mkubwa, lakini kwa vikosi au Wizara na mimi ndio kamanda wao, basi nikaagiza mara moja lirekebishwe hilo. Kwa hivyo, sisi tunakwenda kiaskari na kinidhamu, basi naamini litatekelezwa mara moja. Ahsante.

Nam. 99

Mapande ya Zege Barabara za Mji Mkongwe

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Wananchi wa Zanzibar wamekua wakishuhudia kuwekwa mapande ya zege pembeni mwa barabara nyingi za Mjini hususan eneo la Mji Mkongwe, hatua hiyo inayochukuliwa na Serikali kupitia Baraza la Manispaa na Taasisi nyengine za Serikali inatoa mshangao kwa umma na kusababisha kujiuliza maswali mengi.

(a) Ni taasisi gani inayotoa ruhusa ya kutengeneza mapande haya ya zege, na kuyaweka pembezoni mwa barabara kwa ajili ya kuzuia magari yasiingie sehemu zisizoruhusiwa kama vile eneo la Bandari ya vyombo vya abiria karibu na *Marine Science*.

(b) Kwa sasa yapo mapande mangapi ya zege na Serikali kupitia taasisi husika imetumia kiasi gani cha fedha kutengeneza vifaa hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 99 lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mapande ya zege yaliopo pembezoni mwa barabara ni mali ya Baraza la Manispaa. Mapande hayo yamewekwa kwa ajili ya kuwadhibiti madereva wanaovunja sheria za kuegesha au kupitisha magari barabarani katika sehemu zisizohusika. Juzi nililieleza hili suala. Hapo mwanzo mapande hayo yalitengenezwa na Kampuni ya Skansa, kwa ajili ya kuwekea mabomba ya maji machafu yaliyoelekea pwani, wakati wa utekelezaji wa mradi wa michirizi awamu ya kwanza mwaka 1994 – 1998.

Kwa hivyo, mapande hayo ya zege ni sehemu ya mabaki ya vifaa baada ya kumalizika mradi huo mwaka 1998. Kwa mujibu wa tathmini tuliyonayo idadi ya mapande ya zege yaliyobakia ni kati ya 80 na 100. kwa wakati huu Serikali haikutumia fedha yoyote kutengeneza mapande hayo, ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibumazuri ya Mhe. Waziri nina swali moja tu la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Serikali ina sheria mbali mbali ambazo zinasimamia usalama barabarani. Kuna sheria za barabara na kuna sheria mbazo askari wetu wa barabarani zimewekwa kwa kuwasaidia. Lakini inavyoonekana ni kwamba sheria zote hizo hazifanyikazi, sasa Serikali imeamua kutafuta msaada wa mapande wa zege.

Je, Mhe. Spika, Mhe. Waziri anakubaliana na mimi kwamba sheria zinazohusu usalama barabarani hazitekelezwi na hivyo Wizara yako hivi sasa imeamua ipate msaada wa mapande ya zege.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nafikiri sote tuliomo humu tunakiri kwa sababu tunayaona na tunapita barabarani. Siku hizi ni jambo la kawaida, utakuta mtu anaendesha baskeli bila ya taa, pahala sio ruhusa kupita wanapita, gari linapitishwa mpaka juu ya vidaraja. Wewe unayetembea kwa miguu ukifanya mchezo basi daladala inakufuata huko huko, hili sio jambo linalohitaji miwani kuliona liko wazi kabisa.

Mhe. Spika, mimi nakiri anayoyasema kwamba madereva wetu wengi sheria za barabarani hawazifuati na askari wetu wapo wanajitahidi, lakini ni kidogo. Kwa hivyo, tunajitahidi kwa pamoja, askari wa barabarani, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na sisi tawala za mikoa, ili kuyapitia haya maeneo na kutizama zile sheria ndogo ndogo ziliopo ili anayetembea kwa miguu apate usalama, anayeendesha gari naye apate usalama na kila mmoja wetu apate usalama ili kuweza kuongoza mji wetu uwe na haiba nzuri, hilo ndio lengo. Kwa hivyo, nakubaliana na yeye kwamba tutajitahidi tukae pamoja sote ili tuzipitie hizi sheria tuziweke sawa ili mambo yende vizuri kwa faida ya watumiaji wa barabara wote, ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa mapande mengi yako katika Mji Mkongwe na Mji Mkongwe wa Zanzibar ni mwanachama wa UNESCO kupitia hifadhi ya Mji Mkongwe.

(a) Je, Mhe. Spika, kuwekwa kwa mapande yale haoni kwamba anakwenda kinyume na taratibu za hifadhi ya Mji Mkongwe. Hilo moja.
(b) Mhe. Spika, kwa kuwa wanachama wa hifadhi ya Mji Mkongwe kupitia *UNESCO* ni wengi na ni mara nyingi nchi nyingi zinaiga mazuri. Je, kuwekwa mapande yale ameiga kupitia nchi gani kupitia wanachama wa *UNESCO* katika hifadhi ya Mji Mkongwe, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba yale mapande tumeyawekwa ili kudhibiti mwenendo mzuri wa magari na pia waendesha maskeli na pikipiki. Sasa tukiona mambo yamekaa sawa, yale ni yakuondoka tunayaondosha, hayakai muda wa kudumu. Hilo ni jambo la kawaida hata juzi nilisema.

Mfano, Mhe. Ali Salum, unajua ukiteremka London *Heathrow* pale unakwenda zako *terminal three* basi utaona mapande kuliko haya, tena mengine yana kisu, ukikosea tu basi mpira wako wa gari unauchana. Sio hapo tu, nafikiri viwanja vya ndege vyote tizama, njia zinazokwendea uwanja wa ndege zinaongozwa na mapande yale. Dar es Salaam tu hapo, kiwanja cha Mwalimu Julius Nyerere pia yapo hayo mapande, ni sisi hapa kwetu tu hatuna, sio jambo geni.

Mhe. Spika, unajua madereva wetu wanataka *shortcut*, sasa kwa miji mikubwa ni hatari. Kwa hivyo, zile zinasaidia mwenendo ya magari, lakini mambo yakishakaa vizuri basi yanaondoshwa tu hakuna tatizo, lakini tusaidiane tu kuwaelimisha hawa watumiaji kwamba wasivunje sheria. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, swali langu ni dogo sana la nyongeza. Ilivyokuwa Mhe. Waziri kwa kupitia Baraza la Manispaa wamepelekea kuyaondosha mapande haya katika siku tano zilizopita kwenye eneo la Bandarini.

Je, Mhe. Waziri anatuahidi nini kuyaondoa mapande kama haya katika eneo lililo chini ya iliyokua nyumba la kulelea watoto pale Forodhani ili pia eneo lile liwe ni la kuvutia kama ilivyokua zamani kwenye sehemu ya mbele ya bandari, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba arudie tena sijamsikia vizuri, samahani Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, ilivyokua Mhe. Waziri kama alivyotujibu juzi, kwamba amesaidiana na Baraza la Manispaa kuyaondoa yale mapande ambayo yalikuweko mbele ya bandari inayotumiwa na abiria wanaokwenda Dar es Salaam na kurudi.
Je, yale mapande ambayo yamebakia katika eneo la Forodhani hapa ilipo nyumba ya kulelea watoto, karibu na Mkahawa wa Achipelago. Je, Mhe. Waziri analiahidi Baraza ni lini atasaidia kuyaondoa yale, ili mandhari ya kuvutia eneo lile yarudi kama zamani na pia msongamano unaosababishwa pale uondoke kama ulivyoondoka bandarini, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mjumbe. Mhe. Spika, naomba nieleze kwamba juzi nilizungumza kuwa njia ile tumeifanya iwe ni njia moja tu. Sasa kuna baadhi ya madereva wanavunja ule utaratibu, wanakuja na kutaka kupita wanaifanya kuwa ni njia mbili, kinyume na sheria. Sasa tumeyaweka yale ili kudhibiti hiyo niliyosema wasivunje sheria. Kwa hivyo, tujitahidi

kuelimishana na wewe ndiye Mwakilishi wa Mji Mkongwe. Hivyo, nakuomba tusaidiane ili hii sheria ifuatwe, ikishafuatwa basi hakuna tatizo tutayaondosha mara moja.

Jengine Mhe. Mjumbe, nakuomba kama wewe ni Mwakilishi mimi na wewe leo twende zetu kule tukafanye uchunguzi usiku ili tuyaone yale mambo yanavyokwenda, halafu turekebishe pamoja, ahsante.

Nam. 147

Uvamizi wa Mashamba ya Serikali

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:-

Wizara ya Kilimo na Maliasili inamiliki mashamba mengi Unguja na Pemba, lakini kuna taarifa kwamba baadhi ya mashamba hayo tayari yameanza kuvamiwa na watu kwa ujenzi au kilimo bila kupata ruhusa ya Wizara husika.

(a) Je, suala hili lina ukweli wowote na ni mashamba mangapi yaliyovamiwa.
(b) Je, kwa nini Wizara ilishindwa kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha mashamba hayo hayavamiwi.
(c) Je, Wizara inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba mashamba hayo yanarudi Serikalini.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 147 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli suala la uvamizi wa mashamba ya kilimo lipo na linafanyika kwa sababu mbali mbali ikiwemo matumizi yasiyokua ya kilimo, hasa zaidi kwa ujenzi wa makaazi ya watu na ujenzi wa kazi za miradi ya maendeleo na taifa. Uvamizi huu umefanyika zaidi katika Wilaya ya Magharibi, lakini sasa umetambaa mpaka kwenye Wilaya nyengine. Maeneo ya mashamba yaliyovamiwa ni pamoja na Kizimbani, Kijichi, Kibele kwa Unguja.

(b) Mhe. Spika, Wizara haikushindwa kuchukua hatua za kuhakikisha kua mashamba hayo hayavamiwi isipokuwa mamlaka ya kumiliki na kumilikisha ardhi yote yako chini ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Wizara ya Kilimo na Maliasili inamiliki baadhi ya mashamba ya Serikali yaliyo chini ya Wizara, vikiwemo vituo vya utafiti. Kwa hivyo, suala la mipango ya matumizi ya ardhi yote yanadhibitiwa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

(c) Mhe. Spika, Wizara yangu kwa kuzingatia umuhimu wa ardhi wa uzalishaji wa mazao, inachukua hatua mbali mbali ili kuhakikisha mashamba hayo yanarudi Serikalini, ikiwemo kuwasilisha kesi za uvamizi kwa Wakuu wa Mikoa hasa katika maeneo sugu yaliyovamiwa sana, ikiwemo Kizimbani, Selemu na Kijichi. Pia Wizara imechukua hatua ya kuwapandisha mahakamani na kuwafungulia kesi baadhi ya wavamizi hao.

Mhe. Spika, mikakati mingine inayochukuliwa na Wizara ni pamoja na kuyapima mashamba yaliyo chini ya Wizara na kuyapatia hati miliki kama tulivyoagizwa na Serikali. Aidha, katika kufanikisha hili hadi sasa mashamba yafuatayo yamekwisha kupimwa na yanasubiri kupatiwa hati.

- Maeneo hayo ni Kizimbani, (Utafiti na Chuo cha Kilimo).
- Selemu, Kijichi na Ndijani, Bambi pamoja na Makunduchi, (maeneo ya kilimo na utafiti).

Mhe. Spika, Wizara pia inashirikiana na taasisi nyengine ikiwemo Serikali za Wilaya, masheha pamoja na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati katika kuhakikisha kua maeneo yenye rutuba kwa kilimo basi yanabakishwa kwa ajili ya kilimo. Zoezi kama hili pia linafanyika Pemba kwa kuyapima maeneo ya kilimo yaliyo chini ya Wizara hii kwa lengo hilo hilo la kuwapatia hati miliki.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba uvamizi upo katika mashamba mbali mbali na umeenea

karibu Wilaya zote za Unguja na Pemba. Mimi nilikua nataka kujua uvamizi uliofanywa katika shamba la Mziwanda liliopo Micheweni ni nani alivamia na Wizara imechukua hatua gani mpaka hivi sasa juu ya shamba hilo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, mimi sio mwenyeji sana Micheweni Pemba, lakini shamba la Mziwanda kama sijakosea nadhani ni lile bonde ambalo linalimwa mpunga na hivi sasa linaingia maji. Lakini najua shamba lile limevuka barabara upande wa pili. Kwa hivyo, nasema kwamba Wizara yangu haihusiki na suala la kugawa ardhi, sisi tunashughulika na masuala yetu ya kilimo. Kwa hivyo, ningemuomba suala hili angelipeleka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ili akapata majibu mazuri, ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba Mhe. Mbarouk Wadi Mussa shamba analolizungumza si bonde la mpunga, isipokuwa ni shamba la Mziwana ni la juu ambapo wananchi wa Micheweni walikuwa wakijipatia faida kwa ajili ya kilimo. Kwa hivyo, shamba hilo liliazimwa na Wizara ya Kilimo, kwa ajili ya kupanda michungwa pamoja na shughuli nyengine za kilimo.

Lakini baada ya Wizara ya Kilimo kuhama na kuliacha shamba lile, basi wananchi walirudi kama kawaida na kuchukua mashamba yao kwa ajili ya kulima. Sasa shamba hilo ghafla lilivamiwa na hivi sasa ni shamba ambalo limemilikiwa na Mama Fatma Karume. *(Makofi)*

(a) Je, ni nani aliyemmilikisha Mama Fatma Karume shamba hilo?

(b) Je, kama Serikali inakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuwarejeshea wananchi mashamba yao kwa ajili ya kujipatia faida.

Mhe. Spika, kama unavyojua Micheweni ni sehemu moja ambayo ni ya ukame na shamba lile lilikuwa likiwasaidia wananchi kwa kujipatia riziki zao.

(c) Je, wananchi wamevamiwa na kupokonywa shamba hilo. Sasa ni lini Serikali itasimamia wananchi kwa ajili ya kurejeshewa shamba lao? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, mwenyewe Mhe. Mjumbe katika swali lake alisema kwamba Wizara ya Kilimo walilitumia na baadaye wakarejesha na mwenye dhamana ya kugawa shamba ni Wizara ya Ardhi. Kwa hivyo, aulize swali sehemu hiyo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Je, Mhe. Waziri huoni kuchelewa kupata hati hizo ambapo mashamba mliokubaliana kuwa yapimwe ni kusababishwa watu kuendelea kuvamia?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, nakubali kwamba kuchelewa ni kusababisha watu kuzidi kuvamia mashamba haya. Lakini kwa kuwa tunayapima na tunaweka *rangers* wetu, kwa ajili ya kutizama ili yasiendelee kuvamiwa, basi tunategemea uvamizi utapungua. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nam. 98

Vikundi vya Uzalishaji Chumvi na Samaki Chambani

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Kwanza nampongeza Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa ziara zake za mara kwa mara kwa kuwatembelea Wanaushirika wa Uzalishaji Chumvi na Ufugaji wa Samaki waliomo katika Jimbo la Chambani. Kwa kuwa

wananchi hao wamehamasika sana juu ya uzalishaji wa chumvi na ufugaji wa samaki. Vile vile kwa kuwa wanavikundi hawa wamekabiliwa na vikwazo mbali mbali zikiwemo umaskini na hata kukosa ushauri endelevu wa kitaalamu.

(a) Je, Wizara yako ina mipango gani ya kuwaendeleza kitaalamu wanavikundi hao?

(b) Je, Wizara yako ina utaratibu gani wa kuwatafutia soko wazalishaji wa chumvi, ili waweze kuzidisha juhudi ya uzalishaji?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kwanza naomba kuzipokea pongezi alizozitoa kutokana na Mhe. Waziri huyo kufanya ziara za mara kwa mara katika kuwatembelea wafugaji wa samaki katika maeneo mbali mbali ikiwemo Jimbo lake la Chambani. Vile vile nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Wanaushirika wa Uzalishaji wa Samaki wanakabiliwa na vikwazo mbali mbali vikiwemo umasikini na ukosefu wa utaalamu katika uzalishaji.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 98 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina mipango mbali mbali ya kuwaendeleza kitaaluma wazalishaji wa samaki na mazao mengi ya baharini. Wafugaji huwa wanapatiwa taaluma ya uzalishaji, ili waweze kuzalisha kwa tija.

Wizara inaendesha vikao vya kuwaongezea ujuzi wa uzalishaji kila inapowezekana. Umepangwa mpangilio maalum wa kutoa mafunzo hayo na inapowezekana wazalishaji hupangiwa ziara za kutembeleana, ili wajifunze kwa vitendo na ziara hizi ni ndani na nje ya nchi.

Mnamo mwezi wa Agosti, 2011 jumla ya wananchi 18 wanaojishughulisha na mazao ya baharini walipatiwa fursa ya kwenda China kwa ajili ya kujifunza, kati ya hao akiwemo mmoja kutoka katika Jimbo la Chambani. *(Makofi)*

Vile vile wataalamu wa Wizara kufanya ziara za makusudi za kuwapitia wanavikundi hao kwa nia ya kukagua shughuli zao, pia kuwapatia ushauri wa kitaalamu, ili waweze kuzalisha kwa tija zaidi.

Katika kuwasaidia kupunguza umasikini Serikali kupitia Miradi ya *MACEMP* na *TASAF* imekua ikisaidia juhudi za wanavikundi hawa katika ujenzi wa mabwawa yenyewe ya kufugia samaki pamoja na kuwapatia vifaa mbali mbali.

Hivi sasa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea linafanya upembuzi yakinifu, ambao utaweza kuainisha maeneo ambayo yatafaa kwa ufugaji wa samaki hapa Zanzibar, ili kuweza kusaidiana na wananchi kuendeleza shughuli hizi.

(b) Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi haina mamlaka katika masuala yanayohusu uzalishaji chumvi na masuala haya yako chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili katika Idara ya Maliasili Zisizorejesheka.

Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi itawasiliana na Wizara ya Biashara na Masoko kuhusiana na kuwapatia masoko wazalishaji wa chumvi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuniona mara ya kwanza leo, napenda kumuuliza Mhe. Waziri katika ziara zake alipotembelea mabwawa ya samaki likiwemo Bwawa la Shamiani Mwambe na alichokizungumza ni kusema kuweka Kituo Kidogo cha Utafiti katika Shehia hiyo ya Mwambe.

Je, Mhe. Waziri ni lini ujenzi huo utaanza, ili tutegemee kupata elimu zaidi katika ufugaji wa samaki?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi): Mhe. Spika, ni kweli katika ziara ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi alieleza juu ya nia ya kujengwa kwa Kituo kitakachoshughulikia Utafiti wa Masuala ya Bahari pamoja na mambo ya uvuvi.

Mhe. Spika, sina hakika kama Mhe. Mwakilishi alikuwemo kwenye ukumbi jana, lakini nilijibu kwa kina ni lini kituo hicho kitajengwa. Kwa hivyo, kwa faida yake kama hakuwemo kwenye ukumbi jana, basi ni kuwa mazungumzo yanaendelea kati ya Serikali ya China na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa ajili ya kuandaa *Memorandum of Understanding*, yaani kutengeneza Hati ya Makubaliano.

Kwa hivyo, baada ya kuwekwa sahihi basi utaratibu wa kawaida wa Kiserikali wa kutekeleza miradi utafuatwa na bado haijaainishwa kwamba kituo hicho kitajengwa katika eneo ambalo yeye amelitaja, kwa sababu Serikali itafanya utafiti kuona hasa ni pahala gani patakua pazuri zaidi katika kujenga Kituo hicho cha Utafiti. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali ya Mwaka 2012

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kutuongoza vyema katika shughuli zetu za Baraza kwa hekima na busara kubwa. *(Makofi)*

Aidha napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali.

Mhe. Spika, baada ya kukushukuru wewe naomba nichukue fursa hii kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako hili tukufu kwa kuupitia mswada huu kwa kina na kutupa maelekezo mbali mbali, ambayo yalisaidia kufanya masawazisho katika mswada huu.

Mhe. Spika, niseme kwamba baada ya kuleta mswada huu na kupitiwa na kamati, tulipata maoni ya wadau ambayo yalitanabahisha kwamba kuna jambo la muhimu sana katika mswada huu, ambalo ni vyema likazingatiwa na kufanyiwa marekebisho. Kwa kweli nashukuru sana Mhe. Spika, baada ya kupata maoni haya serikali iliyatafakari na ikaona ni ya umuhimu sana.

Vile vile Mhe. Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi na afisi yako pamoja na Afisi ya Katibu kwa kutusaidia miongozo ya namna ya kushughulikia maoni haya muhimu ambayo tumeyapata.

Sasa baada ya mazingatio hayo pamoja na maelekezo mbali mbali tuliyopata nikuombe Mhe. Spika kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 85 utupe fursa mswada huu tuurejeshe mswada huu kwenye kamati inayohusika, ili tupate kuzingatia maoni hayo ambayo yametolewa na baadaye tuulete tena mswada huu kwa ajili ya kuja kuujadili. Mhe. Spika, naomba uturuhusu kufanya hivyo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, anachoeleza Mhe. Mwanasheria Mkuu ni kwamba kumetokea jambo ambalo kwa maoni yao ingefaa kurudi tena kwenye kamati, ili kuzingatia hayo maoni waliyopata na hatimaye kupata wasaa wa kuwasilisha mswada huu pamoja na maoni yale yamezingatiwa, wameona ni vyema warudi wakaangalie kwa pamoja na kamati juu ya maoni hayo, kwa kifupi tu mswada hivi sasa hauko tayari.

Waheshimiwa Wajumbe, mimi baada ya kupata taarifa hiyo kwamba mswada hauko tayari, basi nilielekeza kwamba tusifanye-*rush*, kwani ni vizuri kuleta kitu Barazani ambacho kimekamilika na kiko vizuri. Kwa kuwa kumetokea jambo hilo na Kamati ilikuwa imezingatia kwa mujibu wa mswada ulivyokuwa mwanzo na hivi sasa kuna mambo yameingia, basi ni vizuri wakarudi na kwenda kufanya hiyo kazi.

Kwa hivyo, mswada huu haui *withdrawn*, isipokuwa haujakamilika. Kwa maana hiyo, hii ni kukubali tu kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu akakae na Kamati kwa ajili ya kuzingatia upya haya yaliyojitokeza, ili hatimaye tupate

kitu ambacho kitakuwa kina usahihi hapo baadaye. Kwa kweli suala hili mimi naona ni jambo jema na linafaa tena nalikubali.
Sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Kamati mkakae kwa lengo la kuzingatia yaliyotokea, ili mtuletee mswada huu hapo baadaye mkiwa mumeshazingatia marekebisho mbali mbali baada ya kupata maoni hayo ya wadau kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa hiyo, ruhusa imetolewa kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe, kutokana na orodha ya shughuli zetu za leo, maana yake itakuwa hatuna kazi nyengine kwa leo. Kwa maana hiyo, hii inanipa nafasi kusitisha shughuli zetu mara baada ya matangazo mawili matatu, ili tuje wiki ijayo kwa ajili ya kuendelea na kazi zetu.

TAARIFA

Tangazo la kwanza, mara baada ya kuakhirisha kikao hiki Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inawatangazia wajumbe wake wakutane nafikiri chumba kile cha kawaida, kwa ajili ya kwenda kuzingatia mambo mbali mbali yanayohusu kamati hiyo, nafikiria itakuwa yanayohusu huu mswada kama ilivyoelezwa hivi punde kutokana na maombi ya Mwanasheria Mkuu.

Tangazo la pili, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mnaombwa kuhudhuria katika mazoezi ya mpira wa miguu katika Kiwanja cha Mao-Tse-Tung kila siku ya Alhamis, Ijumaa na Jumamosi kuanzia saa 12:30 za asubuhi kwa ajili ya kujitayarisha na mechi kwa wageni wetu wa Arusha *Wazee Sport Club* pamoja na kujiandaa na Mashindano ya Mei Mosi.

Waheshimiwa Wajumbe, tunategemea kwa kujitayarisha hivyo timu yangu hii nzuri, safi itafanya vizuri zaidi katika mechi zote hizo mbili na kutwaa makombe ambayo yametayarishwa kwa ajili hiyo, yaani Kombe la Arusha *Wazee Sport Club* tukicheza na ndugu zetu hao pamoja na lile la Mei Mosi. Kwa hivyo, tuhudhurie mazoezi hayo sote na nikisema sote ni pamoja na mimi, mwisho wa matangazo. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo sasa nasitisha shughuli zetu na kuahirisha kikao hiki hadi siku ya Jumatatu tarehe 02/04/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 5:14 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 02/04/2012 saa 3:00 asubuhi)